



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO  
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**



**MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MEI, 2019 NA MWELEKEO WA  
JUNI, 2019**

**Dondoo za Mei, 2019**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Mei, 2019 na mwelekeo wa viashiria vya mvua pamoja na hali ya joto kwa mwezi Juni, 2019 nchini.

- a) Katika kipindi cha mwezi Mei, 2019 maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata vipindi kadhaa vya mvua hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi. Aidha, Ongezeko la joto la bahari eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilisababisha ongezeko la mvua katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei hususan katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na pwani ya kaskazini.
- b) Mvua za 'Msimu' zimeisha kama ilivyotarajiwa katika wiki ya nne ya mwezi April, 2019 na ya kwanza ya mwezi Mei, 2019. Hata hivyo, maeneo machache ya pwani ya kusini, kusini mwa mkoa wa Morogoro, Kati pamoja na nyanda za juu kusini magharibi yaliendelea kupata vipindi vichache vya mvua zilizo nje ya Msimu katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei, 2019.
- c) Hali ya joto la chini ya wastani kwa kipindi cha mwezi Juni inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.
- d) Vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wote wa pwani mwa nchi.

**1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2019.**

Mvua za Masika zimeendelea kunyesha vizuri katika mwezi Mei, 2019 katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na kanda ya ziwa Victoria). Aidha, Ongezeko la joto la bahari eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilisababisha ongezeko la mvua hususan katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei, 2019 katika

maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na pwani ya kaskazini. Hata hivyo, maeneo machache ya pwani ya kusini, kusini mwa mkoa wa Morogoro, Kati pamoja na nyanda za juu kusini magharibi yaliendelea kupata vipindi vichache vya mvua zilizo nje ya msimu katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei, 2019.

## **2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2019**

### **2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa katika eneo la Kitropiki la Bahari ya Pasifiki, mashariki mwa Bahari ya Hindi pamoja na maeneo ya kati Kusini mwa Bahari ya Hindi. Hali kadhalika, joto la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola katika kipindi cha mwezi Juni, 2019. Aidha, hali hii ya joto la juu ya wastani katika bahari ya Hindi inatarajiwa kusababisha uwepo wa mvua za nje ya msimu katika maeneo machache ya ukanda wa pwani. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuimarika na hivyo kusababisha vipindi vya upepo mkali pamoja na hali ya ubaridi katika maeneo mengi ya nchi.

### **2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2019**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya kanda ya ziwa Victoria pamoja na ukanda wa pwani katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Juni, 2019. Aidha, hali ya joto la wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, vipindi vya baridi vinatarajiwa hususan nyakati za usiku na alfajiri. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

#### **2.2.1 Maeneo Yanayopata Misimu Miwili ya Mvua kwa Mwaka**

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**

Vipindi vichache vya mvua nyepesi za nje ya msimu vinatarajiwa hususan katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba katika wiki ya kwanza ya mwezi Juni, 2019 ikifuatiwa na hali ya ukavu. Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 22 hadi 26 katika maeneo mengi. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya miinuko ya mkoa wa Tanga hususani wilaya za Lushoto na Bumbuli zinatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 20.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 hadi 24 katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 18. Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 hadi 18 katika maeneo mengi. Haya hivyo maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 14. Vipindi vichache vya mvua nyepesi za nje ya msimu vinatarajiwa hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi.

### **2.2.2 Maeneo Yanayopata Msimu Mmoja wa Mvua kwa Mwaka**

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 hadi 18 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 24 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 hadi 14 katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko pamoja na mkoa wa Njombe yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8. Maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini cha joto cha juu ya nyuzi joto 14. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi, ingawa kuna uwezekano wa vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko (Tukuyu na Njombe).

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 20 hadi 24 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea.

#### **Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 20 hadi 24 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko ya mkoa wa Ruvuma yanatarajiwa kupata chini ya nyuzi joto 20 katika kipindi cha mwezi Juni, 2019. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea.

## **2.2 MATARAJIO KWA MWEZI JULAI, 2019**

Kwa ujumla kwa kipindi cha mwezi Julai, 2019 hali ya ukavu itakayoambana na vipindi vya baridi inatarajiwa katika maeneo mengi nchini.

Imetolewa na;

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**